

1. UTANGULIZI

Jinsi ya Kutumia Masomo Haya Ya Mafunzo

Tafadhali soma barua hii kabla ya kuanza kutumia masomo haya. Maelezo haya yatakusaidia kutumia zana zetu vizuri zaidi.

Rafiki mpendwa,

Salaam kwenu nyote mnaofundisha katika huduma ya watoto au vijana ama mnaotaka kujifunza kufanya vile. Jina langu ni Mama Lorella, Mkurugenzi Mshiriki wa Kimataifa pamoja na mume wangu katika **Huduma Kwa Kila Mtoto (Every Child Ministries)** Ninaamini kitabu hiki kitakuwa msaada kwako. Nilikiandika kwa sababu nina shauku kuona wewe unanza kuwafikia na kuwafundisha watoto wanaokuzunguka katika mazingira yako, kanisa lako, na kijijini pako ili kwamba wapate kulijua neno la Mungu.

Je Utatumiaje Masomo Haya?

Katika kitabu hiki, sisi katika **Huduma Kwa Kila Mtoto (ECM)** tunakuomba mambo matatu:

1. Kwanza, soma somo kwa uangalifu na makini sana.
2. Pili, fikiria juu ya kile unachosoma.
3. Tatu, andika maoni kwa kila swali tunalokuuliza.

Mara kwa mara utaona mstari kama huu.....au _____. Kila wakati uonapo mstari kama huo simama kusoma. Fikiria kuhusu swali tunalokuuliza. Andika maoni yako katika kitabu hiki. Baadaye unaweza kuanza kusoma tena. Mara nyingi utaweza kuona ni jinsi gani maoni yako yanavyolingana na mawazo yetu. Kila mwisho wa sura tunakutaka kupitia mafundisho ya msingi uliyokuwa unasoma. Pia tunakutaka kufanya mazoezi. Lengo sio tu ujifunze ukweli wa mambo na mawazo. Lengo letu ni kwamba UJIFUNZE MAWAZO na UFANYE MAZOEZI YA KUYATUMIA: Hii itatufurahisha ukifanya hivyo!

Iwapo utakuwa unafuata kitabu hiki katika semina ya mafunzo au darasani, inakupasa kuzifanya sura katika mpangilio wowote ule ambao mwalimu wako ataziwasilisha. Endapo utajifunza katika kitabu peke yako, basi jifunze sura moja au mbili kila wiki. Anza mara moja kufanyia mazoezi mawazo unayojifunza. Ingawaje unaweza ukawa hujajua kufanya kila kitu, fanya bidii kufanyia mazoezi vile vitu ambavyo unavielewa. Kila wiki utapata uelewa mpya na kuongeza dhana na mbinu mpya. Kila wiki ufundishaji wako utaboreka zaidi. Muda utakapokuwa umemaliza kitabu hiki yakupasa kuwa tayari kuwafundisha watoto kwa kushirikiana na kanisa lako. Ni vema mara kwa mara kupitia sura moja au mbili tena ili kujikumbusha yote uliyokwisha kujifunza. Waweza pia kupitia sura zozote zile kuhusu mambo unayoona magumu katika uzoefu wako wa kufundisha. Jaribu nyakati zote kufanya ufundishaji wako kuwa bora zaidi na zaidi.

Iwapo umekuwa mwalimu wa watoto au vijana, fahamu wazi kuwa unalitumikia kanisa la Yesu Kristo. Kama mwalimu wa Shule ya Jumapili au kiongozi fulani wa vijana, wewe sio mfanyakazi wa **Huduma Kwa Kila Mtoto (ECM)**. **Huduma Kwa Kila Mtoto** ni mtumishi tu wa kanisa anayesaidia katika maeneo mahsusi ya kuwafundisha viongozi na walimu na kuendeleza na kusambaza zana za kufundishia. Kila kanisa lina mamlaka juu

ya shule yao ya Jumapili na juu ya mipango yote ya vijana wao. **Huduma Kwa Kila Mtoto (ECM)** haina mamlaka hayo. Jitahidi kuwatii na kuuheshimu uongozi wa kanisa lako kwa kuwa wamechaguliwa na Mungu kuwaongoza watu wake. Taarifa zako za Shule ya Jumapili ni lazima ziende kanisani kwa sababu Shule ya Jumapili ni huduma ya kanisa.

Endapo walimu wa kutosha watakuwa wamefunzwa kijini pako au kanisani pako, unaweza kushauriana na viongozi wa kanisa lako juu ya uwezekano wa kuwatumia baadhi yao kuanzisha vikundi vya mashina katika maeneo yaliyo mbali. Mungu atakuwa hatukuzwi sana iwapo katika maeneo fulani watu hawajifunzi neno la Mungu kwa sababu watu wote wa Mungu wamelundikwa pamoja na wamebaki katika eneo moja.

Mungu na akubariki na kukusaidia katika kazi hii kubwa! Katika siku ile utakayosimama mbele za Yesu Kristo, na iwe watoto wengi waonekane wakikufuata wewe kule wakisema “Tupo hapa mbinguni kwa kuwa tulitubu dhambi zetu na kumpokea Kristo kama mwokozi kupitia mafundisho yako!

Rafiki yako, Mama Lorella.